Na ufadhili wa

Federal Ministry
for Economic Cooperation
and Development

Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Londiani, 2018–2022

Kenya Forest Service

Center for International Forestry Research (CIFOR)

Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Londiani, 2018–2022

Kenya Forest Service

Center for International Forestry Research (CIFOR)

© 2018 Center for International Forestry Research

Yaliyomo katika kitabu hiki yako chini ya leseni ya Creative Commons Attribution (CC BY 4.0), http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

Kenya Forest Service. 2018. *Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Londiani, 2018–2022*. Bogor, Indonesia: CIFOR.

CIFOR
Jl. CIFOR, Situ Gede
Bogor Barat 16115
Indonesia

T +62 (251) 8622-622
F +62 (251) 8622-100
E cifor@cgiar.org

cifor.org

Tungependa kuwashukuru wafadhili wote ambao waliunga mkono kazi hii kupitia michango yao kwenye Mfuko wa CGIAR: https://www.cgiar.org/funders/

Maoni yoyote yaliyotolewa katika chapisho hili ni ya waandishi. Haipaswi kuwakilisha maoni ya CIFOR, wahariri, taasisi za waandishi, wafadhili wa kifedha au wachunguzi wa chapisho.

Yaliyomo

1 Utangulizi **1**

1.1 Umuhimu wa mpango huu 1

1.2 Mchakato wa uandalizi wa mpango 1

2 Msingi wa mpango wa usimamizi **3**

2.1 Thamani ya hifadhi ya msitu 3

2.2 Matishio kwa uhifadhi wa msitu 3

2.3 Vikwazo katika uhifadhi wa msitu 3

2.4 Uchambuzi wa tatizo 3

2.5 Mtazamo ya mpango 4

2.6 Lengo kuu 4

3 Usimamizi na Utumiaji wa Msitu **5**

3.1 Ugawaji kanda za msitu 5

4 Programu za Usimamizi **7**

4.1 Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu Asilia 7

4.2 Programu ya Kuendeleza Mashamba ya Msitu 8

4.3 Programu ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji 10

4.4. Programu ya Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii Ikolijia 10

4.5. Programu ya Maendeleo ya Jamii 10

4.6 Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Vifaa 10

4.7 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Wati 12

4.8. Programu ya Usimamizi wa Ulinzi na Usalama 14

4.9. Programu ya Kuendeleza Elimu na Utafiti 14

Orodha ya jedwali

Jedwali la 1: Uanachama katika vyama na jinsia 2
Jedwali la 2: Vigezo vya kugawa kanda za msitu 5
Jedwali la 3: Shughuli za usimamizi za Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu Asili 8
Jedwali la 4: Shughuli za usimamizi za Programu ya Kuendeleza Mashamba 9
Jedwali la 5: Shughuli za Usimamizi za Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji 11
Jedwali la 6: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Wanyamapori na Utalii Ikolojia 12
Jedwali la 7: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Jamii 13
Jedwali la 8: Shughuli za Usimamiaji wa Programu ya Miundombinu na Vifaa 14
Jedwali la 9: Shughuliz za Usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Watu. 15
Jedwali la 10: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Kusimamia Ulinzi na Usalama 15
Jedwali la 11: Shughuli za Usimimizi wa Programu ya Kuendeleza Elimu na Utafiti 16

Orodha ya vielelezo

Kielelezo 1: Mamlaka ya usimamizi wa CFA 2
Kielelezo 2: Ramani ya ugawaji wa hifadhi ya Msitu wa Londiani 7

Ufupisho

Msitu wa Londiani ni miongoni mwa misitu mingi katika Kaunti ya Kericho. Msitu huu una eneo la hekta 9,015.50. Msitu ulitangazwa katika gazeti la serikali kupitia taarifa ya kisheria nambari 44 ya 1,932 kwa lengo ya kuuhifadhi. Ofisi ya msitu inapatikana katika kaunti ndogo (subcounty) ya Londiani katika Kaunti ya Kericho na inapakana na wilaya (division) za Chepseon na Kuresoi. Msitu umegawanywa katika viunga vitatu—Kedowa, Chebewa na Londiani—ambavyo pia vimegawanwa katika safu ya vitalu kwa urahisi wa usimamizi. Msitu wa Londiani unasimamiwa na meneja pamoja na watumishi husika wa KFS wakichangia katika usimamizi. Mhifadhi bonde ya Kaunti ya Kericho pia ana ofisi ndani ya msitu wa Londiani. Msitu uko karibu takriban mita 2,326 kutoka usawa wa bahari. Msitu huu ni kati ya misitu ya kwanza ambayo Mpango wa Uendeshaji Shirikishi wa Msitu (PFMP) uliendelezwa baada ya Sheria ya Misitu ya 2005 kupitishwa na kutekelezwa mwaka 2007. PFMP iliyotangulia ilizinduliwa mwaka 2012 na mkurugenzi wa Kenya Forest Service (KFS) na ilikuwa ya muda wa miaka mitano hadi Desemba 2016. Mwongozo wa PFM unahitaji kuwa miezi 6 kabla ya kukamilika kwa mpango huo, mchakato wa kupitiwa mpango unapaswa kuanza ili kuhakikisha kuwa mpango huo unafanyika kabla ya kikomo cha mhula. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha, mchakato wa mapitio haukuanza hadi Oktoba 2017.

PFMP hii inatokana na mapitio ya rejea, rekodi ya rasilimali, savei ya bioanuwai, savei ya kijamii na ya kiuchumi, savei za eneo na majadiliano ya wazi, na ushirikiano na wanajamii jirani wa msitu na wadau wengine. Mchakato wa uendelezi wa mpango ulijumuisha mapitio ya mpango uliopita. Mpango huo ulianzishwa na Kamati ya Mapitio ya Mpango wa Mitaa yenye wajumbe 16: 10 kutoka LOCOFA, 1 kutoka WRUA, 1 kutoka KWS, 1 kutoka Wizara ya Udhibiti wa Mambo ya Ndani, 1 kutoka KEFRI na 2 kutoka ofisi ya KFS Londiani (wanaume 11 na 5 wanawake) chini ya mwongozo wa washauri.

Dira ya Msitu wa Londiani ni “Kuwa msitu uliohifadhiwa kwa hali ya juu zaidi katika Mau Conservancy”. Dhima ni “Msitu uliyohifadhiwa na kusimamiwa kwa hali ya juu na matumizi yake yakiwa endelevu.” Lengo kuu la mpango huu wa usimamizi ni “kuimarisha shughuli za msitu kwa utoaji wa bidhaa na huduma za mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo”. Ili kufikia lengo na madhumuni yaliyowekwa, mpango huu unapendekeza kufanya programu tisa za usimamizi: i) Usimamizi wa uhifadhi wa misitu ya asili, (ii) Uendelezaji wa mashamba, (iii) Usimamizi wa rasilimali ya maji, (iv) Wanyamapori na utalii ikolojia, v) Maendeleo ya jamii, vi) Utafiti na Elimu, (vii) Ulinzi na usalama, (viii) Kuendeleza miundombinu, na (ix) Kuendeleza rasilimali watu.”

Utekelezaji wa mpango huu kwa miaka 5 ijayo, gharama inakadiriwa kuwa shilingi za Kenya milioni moja na thelathini na nne (KES 134 milioni). Bajeti ya kila programu na shughuli itakayotekelezwa imeandikwa kivyake. Inatarajiwa kwamba mwishoni mwa kipindi cha miaka mitano, ikiwa mpango utatekelezwa kwa uangalifu, rasilimali za Msitu wa Londiani na maeneo yake ya karibu yatahifadhiwa vizuri na kutumiwa kwa njia endelevu itakayoboresha maisha ya jamii wa maeneo jirani wa misitu na wadau wengine, na hasa kwa watu **2,505** (wanaume 1023, wanawake 920, vijana 462, watu wenye ulemavu 25) wanachama wa

CFA, baadhi yao pia ni wanachama wa vyama vya watumiaji wa rasilimali maji (WRUA).

PFMP hii inazingatia jukumu la misitu katika utoaji wa bidhaa na huduma za mfumo ekolojia. Hasa, inashirikisha WRUA katika mchakato wa mipango na shughuli kwa pamoja kati ya WRUA na CFA. Aidha, mpango huo unachukua hatua maalum za kushirikisha masuala ya jinsia katika mchakato wa uandaaji wa mpango huu na ikajumuisha mtaalamu wa jinsia katika timu ya uandaaji.

Sura ya 1

Utangulizi

1.1 Umuhimu wa mpango huu

Mpango wa usimamizi shirikishi wa msitu wa Londiani, Londiani PMFP, unaendelezwa kutimiza mahitaji ya Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu 2016, Sehemu 47 (1) na 48 (4). Sehemu ya 47 (1) inaeleza kwamba "Kila msitu ya umma, hifadhi ya asili na msitu wa muda utasimamiwa kwa mujibu wa mpango wa usimamizi unaozingatia mahitaji yaliyoodhoreshwa na kanuni zilizopendekezwa na Katibu wa baraza la mawaziri. Kifungu cha 48 (4) kinaelekeza ifuatavyo: "Pale ambapo huduma ya ruzuku inatoa ruhusa kwa mujibu wa kifungu hiki, inaweza kuweka masharti kama inavyoonelea ikiwa ni pamoja na uandaaji wa mpango wa usimamizi wa msitu kulingana na Sheria hii."

Andiko hili ni muhtasari wa PMFP na lengo lake nikuhakikisha kuwa mipango mikuu ya miradi ya usimamizi wa programu ambayo wanachama wa Londiani Community Forest Association (CFA) wameipatia kipaumbele kwa kipindi cha miaka mitano 2018–2022 inapatikana kwa urahisi.

Upokeaji na utumiaji wa mipango shirikishi ya usimamiaji umekuwa njia moja ya kuafikia usimamizi bora, wenye ufanisi na tija zaidi wa maeneo ya misitu. PFMP iliyopitiwa inalenga kupunguza migogoro kati jamii majirani wa misitu na wadau wengine, na hivyo kuwapa fursa ya kuchangia kwa usimamizi endelevu wa misitu na kusaidia jamii za vijijini kujitafutia kipato kupitia misitu kwa njia endelevu. Utekelezaji wa shughuli za uboreshaji endelevu wa maisha kupitia msitu ulioainishwa katika mpango wa usimamizi shirikishi wa Msitu wa Londiani na wadau mbalimbali utaimarisha ustawi wa jamii zinazoishi karibu na msitu.

1.2 Mchakato wa uandalizi wa mpango

Mchakato wa kuufanyia mapitio mpango wa usimamizi ulianzishwa kupitia mikutano ya baraza na mikutano ya kuhamasisha umma. Mkutano wa kwanza pia ulitumika kuuzindua mpango huu na ulifanyika tarehe 7 Novemba 2017. Ulihudhuriwa na watu 44 (wanaume 31 na wanawake 13). Mkutano ulikusanya taarifa juu ya uendelezaji wa PFMP iliopita, ushirikishwaji na uwajibakaji wa jamii, utekelezaji wa PFMP iliopita, mafanikio na udhaifu wa PFMP, ushirikishwaji wa wadau na vitishio kwa na msitu. Wawakilishi wa Kamati ya Mapitio ya Mpango wa Mitaa (LPRC) walichaguliwa mwishoni mwa mkutano wa uhamasishaji na walijumuisha wanachama kutoka kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa msitu ambao wajibu wao ulikuwa ni kuhakikisha kuwa PFMP ilijumuisha maslahi maslahi ya wadau wote na hasa jamii jirani wa msitu. Mkutano pia ulikuwa na lengo la kujenga uelewa wa jamii na wa wanachama wa chama cha msitu wa jamii (CFA) kuhusu haja ya kupitia mpango wa usimamizi wa awali na kuwashirikisha katika mchakato wa kuupitia. Wanachama wa CFA walipewa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu ufanisi wa mpango uliopita na hitilafu zake. Wanachama pia walitoa mapendekezo ya kuboresha mpango mpya kwa manufaa yao wenyewe na ya msitu.

Wakati wa mkutano wa uhamasishaji, jamii waliteua wanachama wawili kutoka kwa jumuiya nne za jamii (CBOs) kuwawakilisha kwenye LPRC. Uchaguzi ulifanyika kwa misingi ya uwakilishi wa haki za watumiaji pamoja na kukuza uwakilishi wa kijinsia na vijana. Wakati wa mkutano wa uhamasishaji, washiriki walihusishwa na mchakato wa kuandaa mpango. Wanachama pia walipewa

Jedwali la 1: Uanachama katika vyama na jinsia

Jina la kikundi cha jamii	Wanaume	Wanawake	Vijana	Walio na ulemavu	Jumla
Tulwap	208	187	115	6	516
Mt. Blackett	339	250	211	9	809
Borop	236	128	82	5	451
Mowlem	340	335	49	5	729
Jumla	1,123	900	457	25	2,505

fursa ya kutoa maoni yao kuhusu viwango mbalimbali vya mafanikio ya mpango uliopita, maeneo ya udhaifu waliyoyaona na njia ambazo zingeweza kutumiwa kuboreshwa mpango.

Tathmini ya kiuchumi kwa eneo lililokaribia msitu wa Londiani ilifanyika Novemba 2017 na LPRC kupitia majadiliano ya vikundi maalum 33 (focus group discussions) na kwa uchunguzi wa moja kwa moja uliofanywa wakati wa mchakato wa kuipitia PFMP.

LONDIANI COMMUNITY FORESTRY ASSOCIATION (LOCOFA)

Mtazamo

LOCOFA inalenga kuwa chama cha kinachoongoza katika uhifadhi wa mazingira na uwezeshaji wa jamii katika usimamizi wa rasilimali asili katika eneo kusini mwa Mau Magharibi.

Dhima

LOCOFA inalenga kuongeza kujenga uwezo na kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika shughuli kuboresha rasilimali asilia na za kujimudu kimaisha.

Dira

"Misitu yetu, Maisha yetu."

Lengo la LOCOFA ni kutekeleza PFMP kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu 2016. LOCOFA inawajibika na usimamizi wa rasilmali asilia kupitia ulinzi, uhifadhi na uratibu wa shughuli za mazingira chini ya mamlaka ya Ofisi ya Msitu ya Londiani, mchango wake mkubwa ukiwa Plantation Establishment and Livelihood Improvement Scheme (PELIS) baadhi ya programu nyingine.

Mamlaka ya usimamizi wa CFA yanaoneshwa kwa Kielelezo cha 1.



Kielelezo 1: Mamlaka ya usimamizi wa CFA

Sura ya 2

Msingi wa mpango wa usimamizi

2.1 Thamani ya hifadhi ya msitu

Msitu wa Londiani una thamani sana kwa jamii jirani wa msitu ambao wanautegemea kama chanzo cha kujitafutia maisha kwani hutoa bidhaa kama kuni, malisho ya mifugo, vifaa vya kushawishi, mimea ya kutoa dawa, matunda pori, asali na nyuki. Msitu pia hutoa huduma zisizohesabika za udhibiti na za utamaduni ambazo zinajumuisha uhifadhi wa viumbe hai, husawazisha hali ya hewa, utalii wa ekolojia, utafiti na za kielimu.

2.2 Matishio kwa uhifadhi wa msitu

Msitu wa Londiani umezungukwa na jamii ya wakulima na idadi ya watu ni 228,000 kulingana na sensa ya 1998. Ukuaji wa idadi ya watu kwa mwaka ni asilimia 2.5. Idadi ya watu inakadiriwa kuongezeka hadi 291,859 mwaka 2018. Kiwango cha wastani cha ardhi ni hekta 0.9 kwa wakulima wadogo wadogo (Chanzo: Volume I–Utafiti wa Msingi wa Kaya, Kericho County, uk. wa 1), na hivyo wanakabiliwa na matishio na shinikizo. Shinikizo hasa hutokana na viwango na mwenendo wa matumizi yasiyoendelevu ya ardhi yatokanayo na ongezeko la idadi ya watu, na hivyo kuongeza mahitaji ya bidhaa za misitu, lakini pia na ongezeko la ukosefu wa ajira, ujuzi duni au usimamizi usiofaa na miundo ya jamii ya usimamizi dhaifu. Kadri rasilimali zinapungua kwenye ardhi binafsi, ndivyo watu wanakimbilia msitu ili kujimudu kimaisha.

Wadau mbalimbali ambao walishiriki katika mchakato wa uundaji wa PFMP waliainisha matishio na shinikizo kwa Msitu wa Londiani kama ifuatavyo:

- utumiaji wa hifadhi ya misitu kwa uvunaji wa bidhaa na huduma mbalimbali, k.m. malisho, nguzo na mirunda ili kukidhi mahitaji ya idadi ya watu inayoongezeka
- uvunaji haramu wa bidhaa za misitu kutosheleza mahitaji ya jamii na miji
- uchimbaji wa rasilimali usio na udhibiti wala uendelevu hasa kwa matumizi ya kibiashara na ya kujikimu kimaisha
- migogoro ya wanadamu na wanyamapori.

2.3 Vikwazo katika uhifadhi wa msitu

Kikwazo kikubwa katika usimamizi wa msitu wa Londiani ni ukosefu wa kamati ya usimamizi wa msitu ya ngazi ya chini ambayo inapaswa kuratibu utekelezaji wa shughuli za mpango. Vikwazo vingine ni pamoja na:

- kiwango duni cha watumishi
- miundombinu duni
- ukosefu wa rasilimali za kifedha za kutosha
- ukosefu wa uwezo wa kutekeleza shughuli zilizopendekezwa.

2.4 Uchambuzi wa tatizo

Usimamizi shirikishi haujatekelezwa kwa ufanisi katika msitu huu, hasa kutokana na rasilimali duni na ukosefu wa nia na uratibu sahihi wa KFS. Kuna haja ya kuhamasisha na kujenga uwezo kati ya wanajamii ili washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopendekezwa. Kwa upande mwingine, KFS inapaswa kukumbatia jukumu la jamii katika uhifadhi wa msitu kwa urahisi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizoainishwa katika mpango wa usimamizi.

2.5 Mtazamo ya mpango

Mtazamo ni kuwa kituo cha misitu kinachoongoza katika uhifadhi endelevu na usimamizi wa msitu nchini.

2.6 Lengo kuu

Lengo kuu ni kuhifadhi na kusimamia kwa njia endelevu msitu wa Londiani kwa kutumia njia bora za usimamizi wa misitu ili kuboresha bayoanuai, vyanzo vya maji na mabonde, na faida ya kiuchumi ili kuongeza manufaa kwa jamii na kwa nchi. Malengo mahsusi ya mpango huu yameelezwa katika programu za usimamizi zilizopendekezwa.

Sura ya 3

Usimamizi na Utumiaji wa Msitu

3.1 Ugawaji kanda za msitu

Tazama Jedwali la 2 na Kielelezo cha 1.

Msitu umegawanya katika kanda maalum za usimamizi pamoja na malengo ya usimamizi.

Jedwali la 2: Vigezo vya kugawa kanda za msitu

Kanda	Vigezo vya kugawa kanda	Malengo
Msitu asilia	• Msitu asilia • Maeneo wazi ndani ya msitu • Maeneo yaliyotengwa kama vyanzo vya maji	• Kulinda misitu yote ya asili • Kulinda maeneo asili wazi ya msitu • Kulinda urejeshaji wa mfumo ikolojia katika hali yake ya asili na uanzishwaji wa upandaji miti maalum katika maeneo yenye miti michache (enrichment planting) • Kuhakikisha uoto utalindwa wakati wa kufunga au kulinda mitambo kama vile nguzo za umeme na mifereji ya maji • Kuthibiti ufugaji katika mazingira ambayo yatastahimili ama katika maeneo ya vyanzo vya maji • Kuruhusu shughuli za kujitafutia kipato ambazo sio za uvunaji au za uchimbaji • Kukuza miundombinu ya utalii ikolojia ndani ya maeneo yote yenye vivutio vya utalii ikolojia kulingana na miongozo ya KFS • Kukata njia za watembea kwa miguu msituni na kwa ziara
Maeneo ya mashamba au ya uzalishaji	• Eneo la mashamba ya msitu • Vitalu vya msitu asili katika maeneo yaliyotengwa ya mashamba	• Kusimamia mashamba yote kupitia mfumo wa kibiashara • Kuanzisha shamba kupitia PELIS • Kuruhusu ulishaji katika mashamba yaliyokomaa ukizingatia idadi ya wanyama inayokubalika • Kuruhusu shughuli mbadala za kujitafutia kipato ambazo zinaendeleza uanzishwaji wa mashamba
Kanda ya kitengo	• Eneo la msitu la pembezoni linalojumuisha ardhi ya jamii	• Kukuza mashamba ya msitu na mashamba ya matunda • Kukuza mapato mbadala kwa kuboresha maisha • Kukuza teknolojia mbadala za nishati na za bei nafuu

Kanda	Vigezo vya kugawa kanda	Malengo
Nyika	• Vitalu vya msitu vilivyo wazi	• Kukuza ufugaji mifugo • Kukuza ufugaji nyuki • Kukuza sekta ya wajasiriamali wadogo
Urejeshaji /Eneo la vichaka	• Maeneo yaliyo na mashamba yasiyostahili kuwa huko • Maeneo ya msitu yaliyo na vichaka	• Kuondoa mashamba ambayo hayaingiani na mfumo wa eneo kwa kuikata miti na kurejesha kupitia kupanda miti asilia • Kuhifadhi maeneo ya nyika asili na kurejesha msitu asilia katika hali yake ya asili kupitia urejeshaji na kupanda miti maalum katika maeneo yenye miti michache

Sura ya 4

Programu za Usimamizi

4.1 Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu Asilia

4.1.1 Utangulizi

Eneo la uhifadhi linajumuisha hekta 4,367.18 za misitu asilia yenye utajiri mpana wa bayoanuai, na maeneo ka kuvutia ya utalii ikolojia, ambayo kwa sasa hutumiwa kuhifadhi viumbe hai, ukusanyaji wa kuni unaothibitiwa kupitia matawi yaloanguka na yale makavu, na kwa malisho. Sehemu ya eneo hili (hekta 500) imeporomoka sana na inahitaji kurekebishwa kwa kupanda miti asilia inayofaa. Mpango unapendekeza kuhusisha jamii ya eneo jirani wa misitu, hasa wanawake na vijana.

4.1.2 Malengo ya usimamizi

- Kurejesha maeneo yaliyoharibiwa katika hali yao ya asili



Kielelezo 2: Ramani ya ugawaji wa hifadhi ya Msitu wa Londiani

Jedwali la 3: Shughuli za usimamizi za Programu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Msitu Asili

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5	CFA/KFS	
Lengo 1: **Kuurejesha msitu asili katika hali yake ya asili (hekta 500)**										
Uzalishaji mbegu ('000')	Na.	500	Miche	50	100	150	150	50	CFA, WRUA, KFS	1.2 milioni
Upandaji	ha	500	Eneo lililopandwa	50	100	150	150	50	CFA, WRUA, KFS	600,000
Upaliliaji	ha	500	Eneo lililopaliliwa	50	150	300	450	500	CFA, KFS	1.55 milioni
Ulindaji msitu ili kuurejesha	ha	500	Eneo lililorejeshwa	50	100	150	150	50	CFA, WRUA, KFS	300,000
Lengo 2: Uhamasishaji uhifadhi wa spishi za mimea ya kipekee										
Uainishaji wa spishi zisizoonekana mahali pengine duniani, zilizo adimu, zilizo hatarini kubwa yakutoweka, na zilizo hatarini	Na.	3	Spishi zilizohifadhiwa	0	1	1	1	0	CFA, WRUA, KFS	200,000
Lengo 3: Kuboresha maisha kupitia mfumo wa PELIS										
Utoaji wa madawa kwa matumizi ya jamii	kg	500	Watakaofaidi	100	100	100	100	100	CFA, KFS	480,000
Urinaji asali	kg	500	Watakaofaidi	100	100	100	100	100	CFA &KFS	480,000
Uvunaji nyasi/malisho	mifuko	1,000	Watakaofaidi	200	200	200	200	200	CFA & KFS	960,000
Ufugaji wanyama ('000')	Na.	3.6	Watakaofaidi	3.6	3.6	3.6	3.6	3.6	CFA	480,000
Ukusanyaji kuni ('000')	Na.	4.8	Hundi	4.8	4.8	4.8	4.8	4.8	CFA	960,000
Uvunaji wa mazao ya msitu yatakayo tumiwa na wajasiriamali wachanga na wadogo k.m. papyrus, liana, matawi yaliyopunguzwa, udongo kwa matofali, etc.	KES	50,000	Watakaofaidi	5	10	10	10	10	CFA	50,000
Uvuvi na kilimo cha samaki	Siku	100	Watakaofaidi	100	100	100	100	100	CFA, WRUA	480,000
Kuongeza thamani mazao ya msitu k.m. asali na madawa kwa matumizi ya jamii	Na.	5	Bidhaa zilizo boreshwa	1	1	1	1	1		6 milioni

- Kukuza uhifadhi wa spishi za mimea ya kipekee
- Kutekeleza shughuli za kuboresha maisha.

4.2 Programu ya Kuendeleza Mashamba ya Msitu

4.2.1 Utangulizi

Eneo la jumla lililotengwa kwa uendelezaji wa mashamba ya msitu ni hekta **3,704.87**; kati ya eneo hili hekta **1,983.05** zimepandwa mashamba ya miti ya kigeni ya msonobari au msindano (pine), cypress na mkaratusi (eucalyptus); **hekta 1,051.46** ya mashamba ya miti ya kigeni ambazo haifai kuwa hapa na mashamba haya yatageuzwa na kurejeshwa kuwa misitu asili, na hafu ya **hekta 619.87** ambayo itapandwa na miti hiyo ya mbao laini kupitia PELIS. Eneo hili kwa sasa linatumiwa kwa mashamba ya misitu ya viwanda na malisho ya kudhibitiwa.

Jedwali la 4: Shughuli za usimamizi za Programu ya Kuendeleza Mashamba

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5	CFA/KFS	
Lengo 1: **Kuanzisha mashamba kupitia PELIS kwenye hekta 430 kwa muda wa miaka 5**										
Uzalishaji wa miche ukijumuisha wanawake na vijana (‘000’)	Na.	8,600	Miche iliyozalishwa	300	200	160	100	100	CFA, KFS	1.72 milioni
Utayarishaji ukijumuisha wanawake na vijana	ha	430	Eneo lililotayarishwa	150	100	80	50	50	CFA, KFS	3.913 milioni
Upandaji ukijumuisha wanawake na vijana	ha	430	Eneo lililopandwa	150	100	80	50	50	CFA, KFS	1.5 milioni
Lengo 2: Matunzo ya mashamba										
Upaliliaji ukijumuisha wanawake na vijana	ha	430	Eneo lililopaliliwa	150	100	80	50	50	CFA, KFS	
Kuongeza nafasi kati ya miti ukijumuisha wanawake na vijana	ha	50	Eneo miti imeondolewa	10	10	10	10	10	CFA, KFS	262,500
Upunguzaji matawi ukijumuisha wanawake na vijana	ha	500	Eneo lililopunguzwa	100	100	100	100	100	CFA, KFS	7 milioni
Upunguzaji miche/miti ukijumuisha wanawake na vijana	ha	500	Eneo lililopunguzwa	100	100	100	100	100	CFA, KFS	4 milioni
Lengo 3: Kuboresha maisha kupitia PELIS										
Ugawaji wa viwanja na wafadhili kuhakikisha ugawaji sawa kati ya wanaume, wanawake na vijana	Na.	5	Rejesta ya PELIS, ramani, idadi ya wanawake katika rejesta	1	1	1	1	1	CFA, KFS	50,000
Mikataba ya masikizano na wanajamii (ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana na vikundi)	Na.	5	Kipato	1	1	1	1	1	CFA	8.750 milioni

4.2.2 Malengo ya usimamizi

- Kuanzisha kwa mashamba ya miti kupitia PELIS
- kutekeleza shughuli za kilimo cha kupanda miti miungoni mwa mazao (silviculture)
- kutekeleza shughuli za kuboresha maisha
- kuendeleza mashamba ya hali ya juu ya miti mbao laini kwa ajili ya kuuza kwa viwanda vya mbao.

4.3 Programu ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji

4.3.1 Utangulizi

Kanda hii ya uhifadhi ni eneo la hekta 4367.18 za msitu asili ambao unajulikana kuwa bonde na chanzo muhimu cha maji (hekta 500 zitarejeshwa kupitia Programu ya Usimamizi wa Msitu Asili).

4.3.2 Malengo ya usimamizi

- Kuboresha uhifadhi wa udongo na maji/na uwezo wa msitu wa kuhifadhi maji
- Kulinda na kuhifadhi maeneo kando ya mito na vijito
- Kuboresha afya ya jamii kupitia usambazaji wa maji safi na salama
- Kuboresha uhusiano kati ya CFA na WRUA

4.4. Programu ya Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii Ikolijia

4.4.1 Utangulizi

Msitu wa Londiani umejaa wanyamapori aina mbalimbali na unao uwezekano wa utalii ikolojia kutokana na kuwepo kwa mazingira ya kuvutia. Shughuli za utalii ikolojia ambazo zilipendekezwa katika mpango wa usimamizi wa awali hazikutekelezwa hasa kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha. Kwa hiyo ilibidi ushirikiano uanzishwe na wadau wengine na wawekezaji ili shughuli zilizopangwa zitekelezwa katika msimu wa miaka tano ijayo.

4.4.2 Malengo ya usimamizi

- Kuhifadhi wanyamapori na makazi yao
- Kuendeleza miundombinu ya utalii ikolojia
- Kulinda aina zilizopo za wanyamapori
- Kukuza utalii wa ndani kwa njia ya utangazaji

4.5. Programu ya Maendeleo ya Jamii

4.5.1 Utangulizi

Jamii zinazoishi katika ukanda wa utelekelezaji na wamiliki wadogo wadogo wenye wastani wa ardhi ya takriban hekta 0.9 (Chanzo: Volume I–Utafiti wa Msingi wa Kaya, uk. wa 1, Kericho County, 2009), na wana kipato cha chini kutokana na ukosefu wa ajira na kilimo kinachotumia mbinu zilizopitwa na wakati. Kaya hupata wastani wa KES 87,858 kwa mwaka na mazao ya mimea yakichangia sehemu kubwa ya kipato hiki (Chanzo: Utafiti wa Msingi wa Kaya, Kericho County 2009, uk. 35). Wengi wa wanajamii wanautegemea msitu kama chanzo chao cha nishati ya kuni, vifaa vya ujenzi na lishe kwa wanyama wao. Kwa hivyo, kuna haja ya serikali ya kaunti pamoja na KFS kuongeza utoaji wa huduma za ugani huko vijijini ili kuhamasisha na kuendeleza utoaji wa ushauri wa kiufundi kwa jamii katika kanda ya kitengo katika maeneo ya msitu, kilimo na shughuli nyingine za kuboresha maisha.

4.5.2 Malengo ya Usimamizi

- Kukuza upandaji miti kwenye mashamba na muundo wa kilimo mseto
- Kukuza matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati safi na jadidifu
- Kusaidia jamii kujikimu kimaisha kupitia shughuli za kuongeza kipato
- Kukuza upandaji wa mimea ya malisho, miti na vichaka
- Kuimarisha utawala wa jamii kupitia kujenga uwezo ili kuwawezesha kupokea na kutumia teknologia mpya za kilimo.

4.6 Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Vifaa

4.6.1 Utangulizi

Msitu unasimamiwa na meneja wa msitu, meneja msaidizi wa msitu na watumishi kutoka KFS. Hali ya jengo la ofisi na nyumba 10 za watumishi inasikitisha na zinahitaji ukarabati. Navyo vifaa vinavyohitajika kutekeleza shughuli zilizopangwa havitoshi.

Jedwali la 5: Shughuli za Usimamizi za Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Kuboresha uhifadhi na utumiaji wa rasilimali za maji										
Kujenga uelewa kuhusu ulinzi wa maeneo kando ya mito na vijito utahusisha maswala muhimu k.m. jinsia, hakimiliki ya miti/ msitu	Na.	20	Mikutano, filamu, michezo	4	4	4	4	4	CFA, KFS, WRUA	1.0 milioni
Kujenga uelewa kuhusu majukumu ya wanawake na vijana katika ushirikishwaji wa uhifadhi na ulinzi wa misitu na maeneo kando ya mito na vijito	Na.	20	Ripoti	4	4	4	4	4	CFA, KFS, WRUA	3 milioni
Tathmini kiasi endelevu cha uvunaji/uchimbaji	mita za mjazo	5,000	Mita za mjazo	1,000	10,000	1,000	1,000	1,000	CFA, WRUA, KFS	2.5 milioni
Utoaji maji	Na.	10	Intake	2	2	2	2	2	CFA, KFS	
Udhibiti wa utoaji wakupita kiasi na utoaji haramu	Na.	5	Ripoti	1	1	1	1	1	CFA, KFS	50,000
Lengo 2: Kulinda na kuhifadhi maeneo kando ya mito na vijito										
Uzalishaji miche	Na.	50,000	Miche iliyozalishwa	10,000	10,000	10,000	10,000	10,000	CFA, KFS, WRUA	1 milioni
Upandaji wa spishi za miti rafiki na maji	km	2.5	Ukanda wa maeneo kando ya mito na vijito uliopandwa	0.5	0.5	0.5	0.5	0.5	CFA, KFS, WRUA	250,000
Lengo 3: Kuboresha maisha										
Usambazaji wa maji kwa kaya	Na.	500	Watakaofaidi	50	150	150	100	50	CFA, KFS, MOW	1.6 milioni
Lengo 4: Kuboresha uhusiano kati ya CFA na WRUA										
Mikutano kwa pamoja kati ya CFA na WRUA	Unit	20	Kumbukumbu ya mikutano	4	4	4	4	4	CFA, WRUA, KFS, WRA	200,000
Kutoa mafunzo ya pamoja kwa wanachama wa CFA na WRUA kuhusu ushirikiano na utawala wa rasilimali za msitu na maji	Unit	10	Ripoti za mafunzo	2	2	2	2	2	CFA, WRUA KFS, WRA	1.0 milioni

Jedwali la 6: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Wanyamapori na Utalii Ikolojia

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Uhifadhi wa wanayamapori na makazi yao										
Utathmini wa msitu	Na.	30	Ripoti	6	6	6	6	6	KWS, KFS, CFA	600,000
Lengo 2: Uendelezaji wa miundombinu ya utalii ikolojia										
Ujenzi wa barabara katika eco-maeneo (eco-sites)	km	53	Ripoti	7	12	12	12	10	KFS	2.12 milioni
Lengo 3: Uboreshaji wa maisha										
Uanzishaji wa mfumo wa usalama / ufuatiliaji wa wageni	Na.	1	Wageni	1					KFS, CFA	240,000
Utoaji wa mawakala wa watalii na wasimamizi	Na.	15	Wageni	3	3	3	3	3	CFA	1.8 milioni
Lengo 4: Kukuza utalii wa ndani										
Kutangaza sekta ya utalii kupitia: - Vipeperushi vya utangazji - Maonyesho ya barabara - Mabango - Magazeti na vyombo vya habari vya kielektroniki - Uendelezaji wa malazi ya kaya (homestay)	Na.	Hundi	Mabango	1	1	1	1	1	KFS/CFA	500,000

4.6.2 Malengo ya usimamizi

- Kuboresha miundombinu ya msitu (barabara, madaraja, jengo la ofisi na nyumba)
- Kutoa vifaa na zana sahihi
- Kutoa nyumba za kutosha kwa watumishi
- Kuimarisha ujulikanaji wa msitu na rasilimali nyingine

4.7 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Wati

4.7.1 Utangulizi

Utekelezaji kwa mafanikio wa programu zote za usimamizi yaliyopendekezwa katika mpango huu utategemea watumishi ambao watasimamia shughuli, ulinzi, usalama wa rasilimali za msitu. Ili watumishi watekeleze kazi zao kwa ufanisi na tija, lazima wawe wa idadi ya kutosha na walio na ujuzi na motisha.

Kituo cha Londiani hakina watumishi wa kutosha ikilinganishwa na wastani wa eneo lake na kazi zinazohitajika kufanywa. Kwa mujibu wa meneja wa msitu, ofisi ya msitu inahitaji kuongeza maafisaa a msitu (forest rangers) 11, wasaidizi 9 na dereva 1.

4.7.2 Malengo ya Programu

Kulingana na hali ya sasa na changamoto zinazozikumba programu hii, mpango huu unapendekeza malengo yafuatayo:

- KFS kuajiri wafanyakazi wa kutosha katika ngazi zote
- kuimarisha utendaji wa wafanyakazi kupitia mafunzo
- kudumisha timu ya wafanyakazi wenye tija
- kuajiri wafanyakazi wa ziada watakapo hitajika

Jedwali la 7: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Jamii

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Kukuza upandaji wa miti kwenye mashamba binafsi ili kufikia asilimia 10 ya uoto										
Uzalishaji wa miche ('000')	Na.	475	Miche	75	100	100	100	100	CFA	7.2 milioni
Kukuza kilimo mseto	Na.	14,200	Wanaofaidi	2500	2700	3000	3000	3000	CFA	100,000
Uanzishaji wa bustani za miti	ha	100	Eneo linalo miti	20	20	20	20	20	CFA	0
Lengo 2: Kukuza vyanzo mbadala vya nishati jadidifu										
Kukuza utumiaji wa teknolojia zinazo tija kwa utumiaji wa nishati	Na.	5	Teknolojia zilizokuzwa	1	1	1	1	1	CFA, MOEP, KFS, NGOs	100,000
Kukuza utumiaji wa teknolojia zinazo tija kwa utumiaji wa nishati	Na.	500	Wanaofaidi	100	100	100	100	100	CFA, MOEP, KFS, NGOs	2 milioni
Lengo 3: Kusaidia jamii kujikimu kimaisha kupitia shughuli za kuongeza kipato										
Kukuza shughuli za kuongeza kipato	Na.	10	Shughuli zilizokubaliwa	2	2	2	2	2	CFA	100,000
Lengo 4: Kuimarisha utawala bora wa CFA										
Uandikishaji upya wa wanachama na usajili wa wengine na kuhakikisha kuwa idadi ya wanawake na vijana inaongezeka	Na.	3,000	Rejesta ya CFA	2,510	2,560	2,700	2,800	3,000	CFA	0
Uanzishaji wa kamati za ngazi ya chini za kusimamia msitu na uwakilishi zaidi au sawa wa wanawake	Na.	**1**	Rejesta na kumbukumbu za mikutano	1						10,000
Uandaaji wa mikutano ya CFA huku taarifa ikitolewa kwa wakati wa kutosha kwa wanachama wote, na kwa wakati na pahali pa mkutano panafaa kwa wanawake	Na.	30	Kumbukumbu za mikutano	6	6	6	6	6		300,000
Kufanya uchaguzi kwa namna ya uwazi ambao unakuza uwakilishaji wa maana wa wanawake	Na.	1	Kumbukumbu za mikutano			1				20,000
Kuendelea na kujenga uwezo na kutoa mafunzo juu ya kutatua migogoro, ushirikishwaji wa jinsia katika maamuzi, ugawanaji sawa wa faida, usimamizi wa fedha na vitabu vya hesabu, uandikaji wa mapendekezo, na kuongeza msaada wa kifedha, n.k. kufikia watu 3,000	Na.	10 (watu 300 kwa kozi	Ripoti za masomo	2	2	2	2	2		150,000

Jedwali la 8: Shughuli za Usimamiaji wa Programu ya Miundombinu na Vifaa

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Kuboresha miundombinu ya msitu										
Kuanzisha kituo cha ziada cha CFA kitakachokuwa na ofisi, chumba cha mkutano, maktaba na mahala pa kuweka vitu	Na.	1	Ofisi			1			CFA	6 milioni
Kuboresha/ kukarabati jengo la ofisi ya msitu na nyumba za watumishi	Na.	11	Nyumba	1	2	3	3	2	KFS	2.5 milioni
Lengo 2: **Kununua vifaa**										
Kununua gari la 4-wheel pamoja na trekta	Na.	2	Vifaa vimenunuliwa		1	1			KFS	10 milioni
Lengo 3: Kuboresha kuonekana kwa msitu na rasilimali zingine (saini na machapisho yanayoelekeza kwa vituo na maeneo)										
Mabango na saini zinazoelekeza kwa vituo na maeneo ya maeneo ya utalii kama vile kaya, mabwawa ya samaki, na maeneo ya kipekee	Na.	6	Mabango	2	2	2	0	0	KFS	300,000

4.8. Programu ya Usimamizi wa Ulinzi na Usalama

4.8.1. Utangulizi

Msitu wa Londiani unaupungufu wa idadi ya watumishi wa usalama ikilinganishwa na wastani wa eneo lake..

4.8.2. Malengo ya usimamizi

- Kuimarisha ulinzi wa misitu na kupunguza shughuli haramu
- Kudhibiti na kuzuia ufugaji katika msitu
- Kufuatilia magonjwa na wadudu
- Kuzuia na kudhibiti moto wa msitu.

4.9. Programu ya Kuendeleza Elimu na Utafiti

4.9.1. Utangulizi

Misitu unaweza kutumika kwa sababu za kuelimisha katika ngazi zote kutoka shule, vyuo, vyuo vikuu na wanajamii.

4.9.2. Malengo ya Usimamizi

- Kufanya utafiti na taasisi husika kuhusu bayoanuai, na tamaduni na matumizi ya kijamii ya msitu
- Kuanzisha kituo cha elimu katika mahabara ya CFA ili kusambaza matokeo ya utafiti
- Kuunganisha ujuzi wa asili katika usimamizi na uhifadhi wa rasilimali asili
- Kuendeleza uwezo wa utafiti wa wakulima na jamii

Jedwali la 9: Shughuliz za Usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Watu.

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Kuhakisha kuwa msitu una idadi ya watumish ya kutosha wa kila ngazi										
Kuajiri, kutawanya au kuhamisha afisa misitu	Na.	11	Rekodi za rasilmali watu	4	3	2	2	0	KFS	12.6 milioni
Kuajiri mtumishi msaidizi	Na.	9	Rekodi za KFS		3	3	2	1		1.9 milioni
Kuajiri dereva	Na.		Rekodi za KFS	1						900,000
Lengo 2: Kuboresha utendaji wa watumishi										
Kupitia mara kwa mara na kuboresha masomo/ kozi yanayotolewa kwa watumishi wa KFS katika ufuatiliaji na tathmini, uimarishwaji wa jinsia, misitu ya jamii/misitu shirikishi, sheria na sera, utatuzi wa migogoro, nk.	Na.	10	Rekodi za KFS za rasilimali watu	2	2	2	2	2	KFS	500,000
Lengo 3: Kudumisha timu ya watumishi wenye motisha										
Kufanya tathmini ya watumishi iliyopangwa kulingana na sera ya rasilimali watu ya KFS	Na.	5	Ripoti	1	1	1	1	1	KFS	100,000
Kubuni njia za kuwazawadi watumishi katika ngazi ya chini na kuwapa motisha	Na.	5	Barua za kusifiwa kwa watumishi ambao wanahitimu zawadi, party za watumishi	1	1	1	1	1	KFS	300,000

Jedwali la 10: Shughuli za Usimamizi wa Programu ya Kusimamia Ulinzi na Usalama

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: **Kuimarisha ulinzi wa misitu**										
Kujenga uelewa wa umuhimu wa kulinda msitu	Na	10	Rekodi	2	2	2	2	2	CFA, KWS, KFS	100,000
Kudumisha mipaka ya msitu, maeneo ya usalama, na uzio la msitu	km	68	Urefu wa msitu chini ya ulinzi na ulinzi unaodumishwa	68	68	68	68	68	CFA, KWS, KFS	2,380,000
Lengo 2: Kudhibiti wadudu na magonjwa										
Kufuatilia uchunguzi wa mapema wa wadudu na magonjwa .	Na		Ripoti za muda	1	1	1	1	1	KFS, KEFRI, CFA	400,000
Lengo 3: Kuzuia na kudhibiti moto wa msitu										
Kuekeleza uchunguzi juu ya moto wa msitu na udhibiti wao	Na.		Ripoti za mara kwa mara	1	1	1	1	1	KFS/CFA	100,000
Lengo 4: Kuthibiti uvunaji wa mazao ya msitu										
Kutunga na kutekeleza sheria ndogo za vikundi vya watumiaji msitu	Na.		Sheria ndogo za vikundi vya watumiaji msitu	1						15,000

Jedwali la 11: Shughuli za Usimimizi wa Programu ya Kuendeleza Elimu na Utafiti

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Lengo 1: Kufanya utafiti kuhusu bayoanuai na matumizi ya kitamaduni na ya kijamii ya msitu										
Kuendeleza ushirikiano na taasisi za utafiti	Na.	4	Barua, makubaliano, mikataba wa makubaliano	1	1	1	1		CFA, KFS, taasisi za elimu na utafiti, NMK	200,000
Kufanya utafiti kuhusu mimea na wanyama wa msitu walio na thamani ya kiuchumi	Na.	2	Ripoti ya matokeo ya utafiti			1	1		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	300,000
Kufanya utafiti kuhusu matumizi ya kitamaduni na ya kijamii ya msitu	Na.	1	Ripoti ya matokeo ya utafiti				1		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	250,000
Kufanya utafiti wa aina za miti inayofaa kwa ajili ya kuanza bustani za miti na kwa kilimo cha mseto	Na.	1	Ripoti ya matokeo ya utafiti				1		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	250,000
Kufanya utafiti wa mbinu sahihi za kurejesha ardhi yenye uharibifu na aina za spishi	Na.	1	Ripoti ya matokeo ya utafiti				1		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	250,000
Kufanya utafiti kuhusa kuongeza thamani mazao mbalimbali ya msitu yasiyo mbao	Na.	1	Ripoti ya matokeo ya utafiti					1	CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	250,000
Kufanya utafiti kuhusu uboreshaji wa maisha	Na.	1	Ripoti ya matokeo ya utafiti					1	CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	250,000
Kusambaza matokeo ya utafiti	Na.	6	Idadi ya mikutano, idadi ya ripoti zilizosambazwa kwa wanachama wa CFA na zinazoonyeshwa katika makavazi ya CFA		1	1	1	1	CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	600,000
Kukuza uhamisho wa ujuzi wa vizazi	Na.	4	Idadi ya mikutano kati ya wazee na vijana, kumbukumbu, na filamu		1	1	1		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	200,000

Shughuli	Kipimo	Shabaha ya miaka 5	Viashiria	Shabaha ya mwaka (miaka)					Wahusika	Bajeti (KES)
				1	2	3	4	5		
Objective 2: Kuanzisha kituo cha elimu katika makavazi ya CFA										
Kunzisha maktaba kwenye makavazi	Na.	1	Rekodi za makhtaba			1			CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	200,000
Makhtaba iwe na vitabu na maandiko mengine ya umuhimu, na ripoti za matokeo ya utafiti	Na.	1000	Rekodi za makhtaba			500	500		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	500,000
Kukuza matumizi ya elimu na ya mfumo ikolojia wa msitu katika shule na taasisi za kujifunza	Na.	8	Vipeperushi na Rekodi ya shule zilizotembelewa				8		CFA, KFS, NMK, taasisi za elimu na utafiti	100,000
Lengo 3: Kuunganisha ujuzi wa asili katika usimamizi wa maliasili na uhifadhi										
Kuweka kumbukumbu ya ujuzi asilia	Na.	1	Rekodi na kumbukumba			1			CFA, NMK, CFA, NGOs	200,000
Ushirikishwaji wa matokeo katika utekelezaji wa mipango ya usimamizi	Na.	1							CFA, NMK, CFA, NGOs	100,000
Lengo 4: **Kuongeza uwezo wa jamii wa kutekeleza utafiti**										
Kuajiri na kuwapatia masomo watafiti wasaidizi kutoka kwa jamii	Na.	4	Rekodi za KFS na CFA			4			CFA, NMK, CFA, NGOs	300,000

RESEARCH PROGRAM ON Forests, Trees and Agroforestry

Utafiti huu ulifanyika na CIFOR kama sehemu ya Programu ya Utafiti wa CGIAR juu ya Msitu, Miti na Kilimo cha mseto (FTA). FTA ni utafiti mkubwa wa dunia kwa ajili ya maendeleo ya kuimarisha jukumu la misitu, miti na kilimo cha mseto katika maendeleo endelevu na usalama wa chakula na kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. CIFOR inaongoza FTA kwa kushirikiana na Bioversity International, CATIE, CIRAD, INBAR, ICRAF na TBI.

Kazi ya FTA inafadhiliwa na Mfuko wa CGIAR: cgiar.org/funders/

cifor.org/water-towers

forestsnews.cifor.org

Center for International Forestry Research (CIFOR)
CIFOR inaendeleza ustawi wa binadamu, usawa na uadilifu wa mazingira kwa kufanya utafiti wa ubunifu, kuendeleza wezo wa washirika, na kushiriki kikamilifu katika majadiliano na wadau wote kuwajulisha sera na mazoea yanayoathiri misitu na watu. CIFOR ni Kituo cha Utafiti cha CGIAR, na inaongoza Programu ya Utafiti wa CGI juu ya misitu, Miti na Kilimo mseto (FTA). Makao makuu yetu ni Bogor, Indonesia, na ofisi huko Nairobi, Kenya, Yaounde, Cameroon, na Lima, Peru.